# MTAALA WA UMILISA

# SEKONDARI MSINGI

## GRED1 7 2024 MUHULA 1

**KISWAHILI** **MASAA 2**

***Mwogozo wa kusahihisha***

| | *Chini ya 40* | *40-59* | *60-79* | *80-100* |
|---|---|---|---|---|
| **PERFORMANCE LEVEL** | *Mbali na matarajio* | *Kukaribia mataraio* | *Kufikia matarajio* | *Kupitisha matarajio* |

**YA MTAHINI**

| **Swali** | **Alama ya swali** | **Alama ya mwanafunzi** |
|---|---|---|
| **INSHA** | | |
| **UFAHAMU** | | |
| **MATUMIZI YA LUGHA** | | |
| **ISIMU JAMII** | | |
| **USHAIRI** | | |
| **JUMLA** | **100** | |

1. Hii ni barua rasmi
   Iwe na sura ifuatayo:
   i. Anwani mbili; ya mwandishi na mwandikiwa
   ii. Sehemu ya maamkuzi; kwa Bw/ Bi
   iii. Mtajo: KUH: YAH: (Kiini cha barua)
   iv. Mwili wa barua Sehemu ya maudhui (Hoja)
   v. Hitimisho au mwisho wa barua
      Mimi wako………
      Sahihi
      Jina
      Baadhi ya hoja za insha
      Visa
   - Wizi

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

- Mauaji
- Matumizi ya dawa ya kulevya
- Unajisi/ubakaji
- Magenge ya majambaz

Mapendekezo

- Kujenga vituo vingi vya polisi
- Mabaraza kufanywa ili kuwashauri wananchi kuepuka maovu/ uhalifu
- Wageni vijijini kuchunguzwa
- Hatua kali kuchukuliwa dhidi ya wahalifu
- Serikali ijishughulishe kumaliza umaskini – kazi kwa vijana/ mikopo ya biashara
- Kuimarisha doria wakati wa usiku n.k

Anayekosa kuzingatia sura ya barua rasmi aondolewe maki 4 baada ya kutuzwa

2.(a) Ufisadi (al.1 x 1=al. 1)

(b) (i) Ajali za barabarani zinasababishwa na kuendesha gari kwa kasi sana
(ii) Kung'olewa kwa vidhibiti mwendo kinyume na masharti ya uchukuzu na mawasiliano.
(iii) Kuwepo kwa magari mabovu barabarani ambayo hayakutimiza masharti ya ukaguzi.
(iv) Ufisadi wa maafisa wa usalama
(v) Barabara mbovu zenye mashimo
(vi) Matumizi ya madawa ya kulevya miongoni mwa madereva wa malori na matrela

(c) (i) Wananchi wafahamishwe ya kwamba wana jukumu la kuwaeleza walinda usalalam endapo gari linapelekwa kwa kasi kupita kiasi.
(ii) Wananchi waelimishwe ili wasikubali kuingia kwenye magari ambayo yamejaa kupita kiasi

(d) (i) Kuwekwa kwa vidhibiti mwendo kwenye magari ya abiria
(ii) Kuwachukulia hatua wale wanaotoa na kuchukua hongo

(iii) Kurekebisha baadhi ya barabara mbovu
(iv) Kuwekwa kwa mikanda ya usalama kwenye magari

(e) (i) Kung'olewa kwa vidhibiti mwen
(ii) Kutokuweko kwa mikanda ya usalama
(iii) Gari kwenda kwa kasi zaidi kutokana na kurekebishwa kwa vidhibiti mwendo ( 2 x 1)

(f) (i) Shida ambayo imedumu muda mrefu bila suluhisho kuliko kiwango kilichokubaliwa
(ii) Mashimo yaliyoachwa baada ya madini kutolewa
(iii) Vifaa vya gari kwenda kwa kasi kuliko kiwango kilichokubaliwa
(iv) Urekebishaji
(v) Kuchukua au kutoa mlungula/rushwa
(vi) Tia hamu ya kufanya jambo (6 x ½ =al. 3 )

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

**SEHEMU YA LUGHA**

3. (a) (i) Chota - chotesha (al.1)
(ii) Lewa – lewesha (al. 1)

(b) (i) King'ong'o – m, n, ny, ng' (yoyore 1x1 =al.1)
(ii) Kiyeyusho – y,w (yoyote 1x1=al.1)

(c) Kwa mfano:-
Kivumishi : Askari shujaa ametuzwa (1x1= al. 1)
Kielezi: Askari yule alipigana kishujaa (1x1=al. 1)
(Hakiki jibu la mwanafunzi)

(d) Vitenzi – tulikwisha, kutambua, alikuwa ndiye (hoja 4 x ½ = al. 2)

(e) Ma(ji) chinjio haya ualikarabatiwa kwa ma(ji) pesa mengi (al. 2)

(f) (i) Kila mmoja aliandika kwa niaba ya mwenzake
(ii) Kila mwanafunzi aliandika kwa sababu ya (al.2)

(g) (i) Uvichanganue (al. 1)

(ii) Kulizibua (al. 1)

(h) Wavu uliookatika ni wao (al. 1)

(i) Kiimbo – Ni upandaji na ushukaji wa sauti unaofanyika wakati mtu anapozungumza (al. 2)
Shadda – Ni mkazo wa silabi katika neno

(k) "Harakisheni mrudi leo, la sivyo mtakosa tuzo" mama alisema (al.2)
au
Mama alisema "Harakisheni mrudi leo, la sivyo mtakosa tuzo".

(l) "Sijaona kitabu kizuri kama "Mayai waziri wa Maradhi," Utaniazima siku ngapi?" Bashiri alimwuliza Rita. (al.2)

(m) Mama anapika na baba akisoma gazeti. (al. 4)

| | |
|---|---|
| S → $S_1$ + U + $S_2$ | $S_2$ → KN + KT |
| S1 → KN + KT | KN → N |
| KN → N | N → baba |
| N → Mama | KT → T+KN |
| KT → T | T → akisoma |
| T → anapika | KN → N |
| U → na | N → gazeti |

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

(n) (i) A – WA (al. 2)
(ii) U – ZI

(o) – wanafunzi watundu- KN
- wanacheza darasani-KT (al. 2)

(p) wa – nafsi
li – wakati
wa – nafsi (mtendewa)
pend – mzizi .shina
eze- kauli/kinyambuzi
a – kiishio 6x ½ = 3)

(q) (i) Nyima mtu uhuru unaohitajika (al.2)
(ii) Kuwa na siri

r) Watalii walivutiwa na chai hiyo (al.2

**4.Isimu Jamii ( al.10)**

a) Ushindani kutoka lugha nyingine kama kiingereza
- Hadhi – Kiswahili kimedumisha
- Athari za lugha ya mama
- Mitazamo hasi kuhusu Kiswahili
- Kutokuwepo kwa sera mwafaka kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa muda mrefu
- Kuhusishwa kwa lugha ya Kiswahili na dini ya kiislamu/ eneo la pwani
- Wamishenari walieneza dini zao kwa lugha ya kiingereza
- Kutokouwa na vitabu vya kutosha vilivyoandikwa kwa Kiswahili
- Uchache wa wataalamu wa lugha ya Kiswahili
- Mkazo wa ufundishaji wa lugha za kikabila katika shule za msingi
- Kuwepo kwa sheria katika shule kuwa Kiswahili kizungumzwe siku moja kwa juma
  Lugha imetengwa katika matumizi ofisini za kiserikali

(zozote 5x2=10 ambazo zimeelezwa)

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

**SEHEMU YA USHAIRI**

**a)** Viongozi wanapovurutana umoja miongoni mwa raia husambaratika

- ingawa raia wanaishi katika hali ya uchochole bado wanashirikiana na kusaidiana kama ndugu
- viongozi huchekelea raia baada ya kuwakosanisha
- viongozi na familia zao hushirikiana pamoja baada ya kugoganisha wananchi
- viongozi wanaendelea na shughuli zao na kuwaacha raia wakizozana wenyewe kwa wenyewe baada ya kuchochea uhasama kati yao
- raia /watawaliwa hukosana kwa mambo madogo yasiyo na msingi wowote`

**(yoyote 1x1=alama 1)**

**b)** -shairi lina beti tano

- mishororo mitano katika kila ubeti
- shairi lina pande tatu yaani ukwapi,utao na mwandamizi
- vina vya ushairi vinahitilafiana katika beti zote isipokuwa vina vya utao vinavyotiririka
- kuna mizani 19 katika kila mshororo mgao wa 8,3,8 isipokuwa kibwagizo chenye mizani kumi na 16
- shairi lina kibwagizo wanapowana fahali ziumiazo ni nyasi **(zozote 5x1=alama 5)**

c) - **mazida**(kurefusha maneno)kwa mfano yawile-yawe, yalikiota-yaliota

- **inkisari**(kufupisha maneno)yali badala ya yalikuwa yendayo-yaendavyo,mepondoka-yamepondeka,hazoshika-hayashika-hayashiki,hazochoka-yasiyochoka, ngali-wangali.
- **Tabdila** (kubadilisha matamshi) ng'ambu-ng'ambo, Hayeshika-hayashiki, mabaku-mabaki
- **Kuboronga sarufi-**ingawa yali dhaifu majani **,**badala ya ingawa majani yalikuwa dhaifu **(zozote 3x1=alama 3)**

**d)** **<u>lugha ya nathari</u>**

japo raia ni maskini walionekana kuwa na umoja,walijitosheleza kwa kusaidiana undugu ulidhihirika miongoni mwao tangu zamani,viongozi walitenganisha raia hawa bila kujali,walipoanza kuvurugana wenyewe viongozi wanapozozana raia ndio wanaoumia.
**(hoja 4x1=alama 4)**

**e)**

mabaka-masalio
kupachana-kufanana **(hoja 2x1=alama 2)**

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes